CHANJO YA COVID-19

# PATA KUJUA UKWELI.

## KAA SALAMA BAADA YA KUCHANJWA.
## LINDA JAMII YAKO.

### Hujalindwa kikamilifu dhidi ya COVID-19 hadi wiki mbili baada ya dozi ya mwisho!

WIKI 2

- Ikiwa ulipewa **chanjo ya sindano mbili**, ni lazima usubiri **wiki 2** baada ya sindano yako ya pili.
- Ikiwa ulipewa chanjo ambayo inahitaji **sindano moja** tu, ni lazima usubiri **wiki 2** baada ya sindano yako.

## KAA SALAMA BAADA YA KUPATA CHANJO

Wataalamu hawafahamu ni kwa muda gani chanjo itakukinga dhidi ya COVID-19 au ikiwa unaweza kueneza COVID-19 kwa wengine baada ya kuchanjwa. Hata baada ya kupewa chanjo, endelea:

- Kuvaa maski.
- Kuhakikisha hukaribiani na watu.
- Epuka mikusanyiko yenye watu wengi.
- Nawa mikono yako mara kwa mara.
- Safisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara

### Hata kama umepewa chanjo kamili, pimwa COVID-19 mara moja ikiwa:

Umekaribiana na **mtu aliye na COVID-19 kisha umeanza kuhisi mgonjwa.** Kaa nyumbani pia mbali na watu wengi.

**Unaishi na watu wengi** na umeingiliana **na mtu aliyeambukizwa COVID-19. Hata kama hujihisi mgonjwa, pata kupimwa.** Kaa nyumbani pia mbali na watu wengi.

NRC-RIM
National Resource Center for Refugees, Immigrants, and Migrants

**Kwa maelezo zaidi: cdc.gov/coronavirus**